



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA



Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na. SHY/MC/F.10/282/16

Tarehe: 24, Machi 2025

**YAH: TANGAZO LA MKOPO WA SERIKALI (ADVANCE LOAN) UNAOTOLEWA NA
HAZINA KWA TUMISHI WA UMMA**

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga inapenda kuwataarifu watumishi wote wa Manispaa ya Shinyanga kuwa imepata mgao wa fedha kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kiasi cha Tshs. 350,000,000/= (Milioni mia tatu na Hamsini elfu tu) kwa ajili ya mkopo wenye riba nafuu asilimia 3 kwa watumishi wa Umma wenye sifa waweze kukopa.
3. Mkopo husika utaombwa kwa njia ya mtandao (on line Application) tofauti na utaratibu ambao ulikuwa unatumika awali na pia mkopo huu hautaombwa kwa njia ya ESS (watumishi Portal). Mtumishi atatakiwa kujisajili kupitia anuani ya mitandao (on line link address) maalumu ambayo ni <https://als.muse.go.tz> au Hazina Portal.

Mambo ya kuzingatia/masharti ya mkopo;

- Mkopaji awe ni mtumishi wa Umma wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga
- Awe na salio la 1/3 ya mshahara
- Mkopaji atalipa "service charge" (Gharama za mkopo au riba ya mkopo) 3% na protection fund (Ulinzi wa mkopo au Bima) 1% kutoka kwenye mkopo huo.
- Hautakopeshwa mkopo mwingine (Top up) kabla ya kurejesha mkopo wa awali
- Utaruhusiwa kufuta mkopo wako wakati wowote kwa utaratibu uliotolewa.

VIWANGO VIPYA VYA MIKOPO YA FEDHA TASLIM

AINA YA MKOPO	NGAZI YA MSHAHARA	KIWANGO CHA JUU CHA MKOPO KINACHOPENDEKEZWA (TSHS).	MUDA WA MAREJESHO
Mkopo wa fedha taslimu kwa ajili ya ununuzi wa Magari, Pikipiki, Samani na matengenezo ya vyombo vya usafiri.	TGS A-C, TGTS A – C, TGHS A – C, AGCS 1 -2, TJS 1 -2, TGOS A – C, TGHOS A – C, SAIS A - C	15,000,000.00	Miezi 72
	TGS D – F, TGTS D – F, TGHS D – F, AGCS 3 -4, TJS 3 – 5, TGRS A – C, SAIS D – F.	30,000,000.00	Miezi 72
	TGS G – H, TGTS G – H, TGHS G – H, AGCS 5 – 6, TJS 6, TGTS D – E, SAIS G - H	40,000,000.00	Miezi 72
	LSSE 1 – 4, TGTS I, TGHS I – J, AGCS 7 – 9, TJS 7 – 9, TGRS F – 1, SAIS I - K	50,000,000.00	Miezi 72
	LSSE 5 – 9, TGHS K – L, AGCS 10 – 12, TJS 10 – 12, SAIS L - Q	55,000,000.00	Miezi 72

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 07.04.2025 saa 9:30 Alasiri.


Revocatus Lutunda

KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA

**MKURUGENZI V/A MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
CHINYANGA**